

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO
(Barua zote zitumiwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Arusha
Simu Namba .027-2535051
Fax Namba. 2535051/2535264



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
S.L.P. 1
LOLIONGO

Kumbi Na NGOR/LD.F.374

Tarehe: 01/08/2008

Kamishna wa Ardhi,
Idara ya Ardhi,
S.L.P. 9230,
DAR ES SALAAM.

**YAH: MAOMBI YA KUBADILI MATUMIZI YA ARDHI SHAMBA
NA 373 LILILOKO KITONGOJI CHA SUKENYA KIJJI CHA
SOITSAMBU WILAYANI NGORONGORO**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Tumepokea maombi toka kwa Tanzania Conservation Ltd mmiliki wa shamba lililotajwa hapo juu. Masharti ya matumizi yaliyoko kwenye hati yao hayana tija kwao na Taifa kwa ujumla hasa kutokana na eneo hilo kuwa karibu na Hifadhi za Taifa, kama vile Serengeti. Hivyo matumizi stahili zaidi ni shughuli za kitalii.

Kama taratibu zilivyo, maombi haya yaliwasilishwa kwenye Kikao cha Huduma za Kiuchumi, Ujenzi na Mazingira cha Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kilichoketi tarehe 23/1/2008 na taarifa kutolewa kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 25/1/2008.

Kimsingi Kikao kilikubaliana matumizi ya shamba hilo yabadilishwe ili litumike kwa manufaa zaidi.

CO/ 231 863
O/S 27/11/08

L.R. 15536

DPP → 2/6/08

Hata hivyo Halmashauri ilipendekeza kuwa wakati kamishna anafanya mabadiliko hayo aone pia kama kuna uwezekanano wa kulipunguza sehemu ili ligawanywe kwa Wanakijiji wa Soltsambu.

Kwa kuwa utwaaji/ufutaji wa miliki kisheria una mchakato wake iwapo kutakuwa na hoja, nashauri mabadiliko hayo yafanyike wakati hoja hiyo inajengwa kwani haina madhara kisheria.

Naomba kuwasilisha.



N.J. Hilli

AFISA ARDHI MTEULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO

Nakala: DED alone kwenye jalada

Viambatanisho:-

- Mihtasari iliyotajwa hapo juu
- Certificate of Incentives
- Certificate of Incorporation
- Barua ya maombi kutoka Tanzania Conservation Limited ya kubadilisha matumizi.
- Land Form No.27.